

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**MKUTANO WA SABA**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA SABA**

**13 APRILI, 2017**

## **MKUTANO WA SABA**

### **KIKAO CHA SABA TAREHE 13 APRILI, 2017**

#### **I. DUA:**

Saa 3:00 Mhe. Job Y. Ndugai (Spika) alisoma Dua na kuongoza Bunge.

Makatibu mezani:

1. Ndugu Ramadhani Issa
2. Ndugu Asia Minja
3. Ndugu Joshua Chamwela

#### **II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Naibu Waziri wa Nchi (TAMISEMI) aliwasilisha:-

- (i) Randama za makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA) kwa mwaka wa fedha 2017/2018;
- (ii) Ripoti ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Taasisi za fedha za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016;
- (iii) Ripoti ya Ukaguzi wa ufanisi juu ya udhibiti wa uendelezaji wa maeneo ya wazi yaliyoainishwa nchini Tanzania;
- (iv) Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi juu ya miundombinu ya Shule za Msingi Tanzania;
- (v) Taarifa ya majibu ya Serikali na mpango kazi wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016.

Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha:-

- (i) Ripoti ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za Fedha za Serikali kuhusu Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016;
- (ii) Ripoti ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016;
- (iii) Ripoti ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za fedha za Mashriki ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016;
- (iv) Ripoti ya jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalum kwa kipindi kinachoishia tarehe 31 Machi, 2017;
- (v) Ripoti ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendkezo ya ukaguzi katika Taarifa Tano za Ukaguzi wa ufanisi zilizotolewa na kusomwa Bungeni kuanzia mwaka 2012 hadi 2013;
- (vi) Majibu ya Hoja na Mpango wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha 2105/2016 Volume I na II (A na B).

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia aliwasilisha Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi juu ya uzalishaji wa wahitimu katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia.

Naibu Waziri wa Nchi (TAMISEMI) kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi aliwasilisha Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi juu ya usalama dhidi ya moto katika majengo ya Umma.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

- (i) Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi juu ya usimamizi wa samani za Barabarani;
  - (ii) Ripoti ya ukaguzi na ufanisi juu ya usimamizi wa kaguzi za vyombo vya majini kwa ajili ya kupewa vyeti vya ubora na kukidhi viwango vya usalama wa usafirishaji.
- Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji aliwasilisha Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa uchukuaji wa maji kutoka vyanzo vya maji.
  - Waziri wa Afya aliwasilisha Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi juu ya usimamizi wa Mikataba iliyoingwa kati ya Serikali na Hospitali binafsi nchini.

### **III. MASWALI**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI)**

Swali Na. 55: Mhe. Josephat S. Kandege

Nyongeza: Mhe. Josephat S. Kandege  
Mhe. Abdallah A. Mtole  
Mhe. Said A. Kubenea

#### **WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

Swali Na. 56: Mhe. Salma Mohamed Mwasu

Nyongeza: Mhe. Salma Mohamed Mwasu  
Mhe. Allan Joseph Kiula  
Mhe. Dkt. Immaculate Sware Somezi  
Mhe. Maulid Said Mtulia

## **WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Swali Na. 57: Mhe. Mbaraka Kitwana Dau

Nyongeza: Mhe. Mbaraka Kitwana Dau  
Mhe. Stephen Hilaly Ngonyani  
Mhe. Ester Amos Bulaya  
Mhe. Riziki Shahari Mugwali

Swali Na. 58: Mhe. Augustino Manyanda Masele

Nyongeza: Mhe. Augustino Manyanda Masele  
Mhe. Sixtus Raphael Mapunda  
Mhe. Pauline Philip Gekul

## **WIZARA YA NISHATI NA MADINI**

Swali Na. 59: Mhe. Lucy Fidelis Owenya

Nyongeza: Mhe. Lucy Fidelis Owenya

### **IV. MATANGAZO:**

1. Wageni waliokuwepo Bungeni walitambulishwa akiwemo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).
2. Mwili wa marehemu Dkt. Macha utawasili Tanzania tarehe 20 Aprili, 2017, utaletwa Dodoma Ijumaa tarehe 21 Aprili, 2017 na maziko yatafanyika tarehe 22 Aprili, 2017.

### **V. KUAHIRISHA BUNGE**

Saa 4:15 asubuhi Spika aliahirisha Bunge hadi tarehe 18 Aprili, 2017 saa 3:00 asubuhi.